***"Yesu Kristo ni Yeye yule, jana leo na hata milele"***
(Waebrania 13:8)

# BARUA YA MUZUNGUKO Juni 1973

Nawasalimu kwa moyo mkunjufu wasomaji wote wa barua hii, kwa jina la Bwana Yesu Kristo, kwa maneno haya ya Warumi 8:14:

***"... kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu."***

Kifungu hiki cha maandiko hakitoi tuumuhimu wa imani kwa Bwana Yesu Kristo, lakini pia inazungumuza juu ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Sisi sote tunahusika namaneno haya, na tunaalikwa kujijaribu wenyewe. Kumekuwa na watu ambao wanasema wanaongozwa na Roho wa Mungu, lakini kujidai tu hilo haitoshi. Vivyo hivyo, siku hizi tunaona harakati tofauti za kidinizajidai kuwa wamepewa Roho Mtakatifu. Wainjilisti nawahubiri pia wanasema wako chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, na kila mmoja hufanya kile kinachoonekana kuwa kizuri kwake, bila kwelikujinyenyekeza kwa Neno la Mungu, na kwa hiyo, wajiachilie waongozwe na Roho Mtakatifu.

Bila shaka watu hawa, pamoja na harakati hiziza kidini, mara nyingi zilianza katika Roho. Lakini sasa matokeo nigani? Kuanza katika Roho haimaanishi kitu kikubwa, ikiwa uongozi wa Roho Mtakatifu hauendelei mpakahatua ya kutufikisha kwenye ukamilifu.

Paulo anatuonya kwa maneno haya: ***"Je! Mumekuwa wajinga namna hii? Baada ya kuanza katika Roho, mnataka kukamilishwa katika mwili?"*** (Gal. 3:3) Kila kitu ambacho niasili ya ki Ungu ni ya kiroho; kwa hivyo, yale yote ambayo watu wanaanza kujiundia wenyewe, hiyo ndiyo mambo ya kimwili. Mmoja anamutenga mwingine, kwa sababu mmoja ametoka kwa Mungu, na mwingine hutoka kwa mwanadamu. Moja huleta uzima, na mwingine, kifo. Kwa sababu: ***"... kwakuwa nia ya mwili ni***

***mauti, bali nia ya roho ni uzima na amani."*** (Rum. 8:6) Ni lazima tutambue kwamba, mbele za Mungu, itastahimili kile tu kilichotungwa na Yeye mwenyewe kwa njia yaRoho wake na kulingana na Neno lake. ***"Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, namininatenda kazi"***. (Yohana 5:17) Hivyo ndivyo Yesu alivyosema, nakatika Wafilipi 2:5 tunapewa onyo hili: "***Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwemo piya ndani ya Kristo Yesu…"*** Yule anayebeba ndani yakenia hizoza ki Ungu yeye daima ni pamoja na tendo la Mungu. 1 Wakorintho 2:14 inasema: ***"Basi mwanadamu watabia yaasli hayapokei mambo ya Roho wa Mungu, maana kwake huyo niupuuzi wala hawezi kuya fahamu, kwakuwa yatambulikana kwajinsi ya Rohoni."*** Kila mtu anaweza kujichunguza mwenyewe, nakujuwa kama anapokea kwa furaha Neno lililofunuliwa na Roho wa Mungu, au kama anampinga. Ikiwa kuna upinzani ndani yetu kuhusu Neno la Mungu hapo nikusema kwamba bado tuna nia za kimwili, nakwamba hatuelewi mambo ya kiRoho. Ikiwa kinyume chaketuna nia za kiroho, basi tutajisikiya furaha ya kilindi na hitaji ya kweli ya kupokea chakulakya kiroho.

## UONGOZI WA ROHO NI NINI?

***"Kwakuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana waMungu."*** (Rum. 8:14) Kwa vitendo, uongozi wa Roho unamaanishakwamba tutambue kile ambacho ni sawa machoni pa Mungu, kwamba tunakiweka kwa matendo, na kwamba kinaonyeshwa kwa wakati unaofaa. Tunapatamfano wazi wa hilo katika Luka 2:25-32. Simeoni alikuwa amepokeaufunuo wa ahadi ya Neno kwa wakati wake, naye akaongozwa na Roho Mtakatifu ndani hekalu: nihapo ambapo aliona kwa macho yake mwenyewe utimilifu wa Neno. Chini yaupako wa Roho, akatmka unabii huu wa ajabu kuhusuYesu.

Tunaona hapa ni nini uongozi wa Roho wa kweli naya kibiblia. Sio utawa ya kujipendeza, lakini ukweli nikutambua ufunuo wa mapenzi ya Mungu na ahadi zake ambayo kwa hiyo

huongozwakwawakati unaofaa namahalipazuri ili kuwa shahidi kuhusu kile Mungu anachofanya. Roho Mtakatifu hatufanyi sisi kupita pembeni yaKristo na ahadi zake. Wote ambao wanaongozwa na Roho wa Mungu wanatambua pia kwa siku zetuutimilifu wa maahadi. Wanakuja kwa Yesu na, wakisukumwana Roho Mtakatifu, wanatangaza kile ambacho kina timilika kulingana naNeno la Mungu. Nao pia, wakiongozwa na Roho wa Mungu wanatambua kazi ya Mungu na kuishiriki.

Kwa kipekee kwenye nafasi za „Injili Kamili“, kunasikilika sana kuhusu uongozi wa Roho Mtakatifu; lakini sisi lazima daima kuchungambele ya macho yetu wazo hili ambalo Roho Mtakatifu anaongoza katika kweli yote. Mutu ambaye kweli kweli anaongozwa na Roho wa Mungu anasema hiyo kwa shida. Yeye hapige tarumbeta mbele yake, lakini popote aendapo huacha alama za baraka. Kuna kitu cha muhimundani yake. Yeye si mupendelevu, wala mutu wamipaka. Hapana, katika uepo yake, kila mtu anajisikia vizuri. Mwenendo wa mtu wa namna hii una elezewa katika Neno kwa maneno haya: ***“… uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.”*** (Wakolosai. 3:3) Ingawa hivyo maisha yake yanafichwa ndani ya Mungu, mishale ya uzima huo haifichwi, yeye, kwa sababu: ***„Kristo, uhai wenu; atakapo funuliwa nanyi pia mutafunuliwa pamoja naye katika utukufu”*** (Wakolosai. 3:4).

Watu wa kweli wa Mungu hawa semi kwa ajili yao wenyewe, na ushuhuda wao hauhusiani na "umimi" wao. Hawawekikwa sehemu ya kwanza mazoezi yao ili wajitukuze, lakini, wanautukuza utukufu wa Bwana, Mungu wao. Ikiwa tunataka kuonekanapamoja na Kristokatikautukufu, lazima tayari adhihirishwe hapa ndani ya maisha yetu. Mungu alifichwa ndani ya Kristo, hata hivyo, kazi za Munguzilidhihirishwa kupitia Yeye. Vivyo hivyo, Kristo, uzima wetu, amefichwa ndani yetu; kwa hivyo, kazi Zake zitadhihirishwa ndani yetu.

***“… wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ndio wana wa Mungu…”*** Katika Agano la Kale na Agano Jipya, tunayo

mifano ya kutosha ya watu walio puliziwa na kuongozwa na Roho wa Mungu. Yesu Kristo, Bwana wetu, anatuonyesha alama yauhakika ya utendaji wa Roho Mtakatifu: ***"…atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu … yeye atawaongoza awatie katika kweli yote … atanena yote aliyo yasikia, na atawaambia mambo yajayo. Atanitukuza, kwa sababu atachukua yaliyo yangu, naye ataiwatangazia…"*** (Yohana 16:8-14) Ni hayo yote ambayo Roho Mtakatifuanazihirisha katika maisha ya mtu anayekuja kwa Kristo na kupokea neema yake. Anaanza kwa kumwongoza kwenye maungamo ya dhambi zake, kwa toba, kwa matengenezo ya makosa yake, na kukubalishwa, kwa kuzaliwa upya, kwa kusafishwa na utakaso, tena kwakumaliza, humjaza Roho Mtakatifu. Mahali kitendo hiki na alama hizi za wazi vinakosa nikusema kwamba kitu fulani si katikautaratibu.

## KIKUNDI CHA KARISMATIKI

Ni kwa usemi huu kwamba tunata Ja leo kitendocha Roho katika maeneo mbalimbali za Ki kristo na makanisa mbalimbali. Inasikilikana ikisemwakwamba, katikamakanisa yote ya Kiprotestanti, kitendo cha Roho Mtakatifu husikia tena upya, na tunaweza kusoma maneno kama vile "Kikundi cha ki Pentekoste katoliki". Wale ambao wanaweza kusoma magazeti ya dinizakigeni wana juwa vizuri kuna nini. Hatutaki kutoa hukumu juu ya hili hapa, lakini tu kuwajulisha ni nini hasa. InasikiKa ikisemwa, na pia kusomeka, ya kwamba watu, katika sehemu nyingi za ulimwengu, wanafanya mazoezi ya ki Pentekoste; nikusema wananena kwa lugha, bila kugeuka kutoka kwamafundisho yote yasiyo ya kibiblia, na bila kuheshimu masharti yakimaandiko.

Kwa hivyo tunapata, katika gazeti la »Logos« ya Marekani (USA), nambari Nov./Des. 1972, ukurasa wa 43, picha ya kupendeza ya mtu ambaye huvuta pipa, ambamo wanaomba kitabo ambacho kina kichwa: «Baba McCarthy anavuta pipa na ananena kwa lugha!». Je, mtu yeyote anaweza kufikiria kwamba Bwana Yesu, au nabii, ao

mtume, amewahi kuvuta pipa? Kwa upande mwingine, tunajua kwamba kuitwa „Baba" ni kinyume na Neno la Mungu, kwa sababu Yesualiwaambia wanafunzi Wake: ***„Wala msimwite mtu baba yenu duniani; Maana Baba yenu ni mmoja, aliye mbinguni.*"** (Mt. 23:9)

Sasa, swali tunalopaswa kujiuliza ni hili: Je, huu ni ubatizo wa kweli wa Kibiblia wa Roho Mtakatifu? Naharakati hii ya sasa ya karismatiki, pamoja na kunena kwake kwa lugha naambapo kila mmoja anaishi katika mapokeo ya kanisa lake, ni sawasawa na Ukristo halisi? Je, Neno la Mungu halisemiwazi: **"*Kwa hiyo tokeni kati yao, muka tengwe nao asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu nami nitawakaribisha nita kuwa baba kwenu nanyi muta kuwa wanangu wa kiume nawa kike, asema Bwana mwenyezi*"**. (2Kor. 6:17-18) Je, Roho wa Mungu hatenganishi zaidi sana leo? na haongozi tenakatika ukweli wote? Je, Roho hatuongozi zaidi kwafundisho la Mitume na manabii?

Safari ya mhubiri mwanamke wa Kipentekoste wa Marekani KathrynKuhlman karibu na Papa alipokelewa vyema katika maeneo yaPentekoste. Swali tunaloweza kujiuliza, hata hivyo, nihii: "Je, kweli ni Roho Mtakatifu aliye muongoza hapo?" Simeoni, yeye, hakuongozwa na Roho mtakatifu kwenda kwa papa, bali alimuongoza kwenda kwa Yesu. Katika gazeti ya "logos"inaonyeshwa kwa Nambari ya Jan/Feb. 1973, ukurasa 32, tunaona muhubiri hu mwanamke wakipentekotiste aki pigwa picha pamoja na Papa, nahapo akamupaMedali ya dhahabu mukononi iliyo maanisha Roho Mtakatifu, hua. Papa anamhakikishia kuwa baraka na maombi yake yangemfuata. Kwake ilikuwaheshima maalum; lakini Yesu anasema nini kuhusu hilo? ***„Mwawezaje kuamini ninyi mnao peyana utukufu ninyi kwa ninyi, nautukufu ule utokao kwa Mungu aliye wakipekee hamuutafuti*?"**. (Yohana 5:44).

Kunawanawakewachache, na wanaume wengi, wanaoshikiliana kampeni za uponyaji zilizofanikiwa, lakini ambazo, wakati huo huowakati, wana hatia ya ukahaba wa kiroho na Roma. Je,

hatukumbuki kile Mathayo 7 inasema, kuhusiana nahiyo? Ingefaa kwa watu kama hao kusoma masharti ambayo waamshi waliojazwa na Roho walimhukumu Papana kanisa la Kirumi!

Gazeti la “Miracle Magazin” laripoti, kwenye ukurasa wa 9, jinsi Billy Graham alichukua nira ya Roma katika chuo cha Kikatoliki “Belmont Chuo”, wakati wa sherehe hiyo ambapo alipokea jina la Daktari Honorisi causa. Kardinali Cushing alitangaza: „Mimi ni asilimia mia kwa mia kwa upande waBilly Graham”. Billy Graham alijibu: „Nijisikiya sawa kuwa nyuma yamitumikiyo ya kanisa katoliki la ki roma kuliko kushikiliana na waprotestanti walio huru”. Je, hii ni lugha na mwelekeo waRoho takatifu? Yesu anasema nini kuhusiana na jambo hilo? “*Kwa maana walipenda utukufuwa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu*” (Yohana 12:43). Hii inatukumbusha pia neno la Ufunuo 13:8: ***“Na watu wote wakao juuya nchi watamusujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu chauzima chamwana kondo, aliyechijwa tangu kuwekwa misingi ya Duniya”.***

Njia ya Wakristo wa kweli haiwapeleki Roma, bali inawatowa roma. Hii ni“ HIVI ASEMABWANA” katika Neno Lake. Yeye Mwenye kupinga hili bado haja elewa nikitu gani. Mamilioni ya Wakristo na ya Wayahudi waliuwawa kwa sababu ya imani yao, kwa sababu hawakutakakukubali imani ya Kirumi. Hapo sasa damu ya wale walio fia imani ina liya Duniani hata Mbinguni, wahubiri wa injili hutafuta njia ya kuletawamini wa wakati huu pole na kuwasafisha boongo iliwapate namna yakuwaongoza tena upya kwenye kifuw cha kanisa katoliki la kirumi. Kama waamini wa wakati huo wangelitambua kile kinacho tendeka mbele yao, wangetoka leo leo katika madhehebu yao na makanisa. Wanawa onyesha vitu kwao kwa njia ya kuvutia sananaile iwafanye kuingiya katika umoja wa madini kwaurahisi. Na hii ndio sababu neno la Mungu linasema: “***Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa…***” (Hosea 4:6). Tayari Isaya alikuwa akisema hivi: ***“Kwamaana waongozao watu hawa ndio wawakoseshao, na hao walio ongozwa na watu hao***

***wameangamiya.*** **"** (Isa. 9:15)

Ninajua kuwa „haionekani vizuri" kuandika kwa njia hii, hata hivyo, ni muhimu kwamba Bwana Mwenyewe asikilikishe neno hii: **"*Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokei mapigo yake…*"** (Ufu. 18:4) Mwito huu sii yawote wote, kwa sababuBwana anasema wazi wazi: ***"… taifalangu …"*** Yeye aliye mali yake atafuata mwito Wake, hiyo ni hakika, kwa maana Bwana alisema hivyo.

## MATUKIO YA WAKATI HUU

Katika wakati wetu, mara nyingi tunashambuliwa na udanganyifu, na asiyekuwa makini hudanganywa kwaurahisi. Mara nyingi, watu wenye hisia nzuri hugeuka kuwa mawindo ya wacha Munguwadanganyifu – na wao wenyewe huwashawishi wengine. Kuna vitendo vinavyotawala wafuasi wao kwa kujifanyakidini, kupitiya ushawishi huo wanaunga mkono maoni yao. Kitendo cha Mhindi Lawrie ni jambo moja katika mengineyo – hizi zinaonyesha ujuzi mwingikwamba hazigunduliki kwa urahisi. Daima ni bora zaidikwanza toa boriti iliyo katika jicho lake, kablaaweze kutoa kibanzi kwenye jicho la nduguye. Wakati wowte kulikuweko wa kina „Yuda" ambao kwanza walitembea na Yesu na waliyokuwa wameitwa naye nakutumikishwa kwa hudma. Siku ikafika Shetani alipoingia ndani yao, na yote yakawa yamekwisha.

Yuda, mpaka siku ile Shetani alipoingia ndani yake, alikuwa mtu mkamilifu. Hivyo ndivyo ilivyo hata kwa wengine, kwa Lawriepia. Huyuwa mwisho alijidai kwamba mnamo Julai 21, 1969, Mungu angekuwa ameingia ndani yake. Hata hivyo, anaonekana kumchanganya Mungu na shetani. Madai yao yasiyo ya kimaandiko na ya makukufuru yanasaliti chemchemu ambako aliwa shota. Wakati anadai kupokea simu ya ndugu Branham mwenyewe, ni njia tu inayopatikana kwakekupata sura fulani ya mamlaka. lakini, kila mwamini anaweza kwa urahisi kutofautisha ma ushuhuda za ndugu Branham – kweli kwa kileambacho Biblia

inasema – madai ya uwongo ya mtu huyo. Pia kuna watu wengi ambao, kwa upande mmoja, madai ya Kristo, lakini ambao, kwa upande mwingine, hawafanyi kile alicho agiza kufanya.

Wengi hujilinganisha na mtume Paulo, na bado wao hawa fundishe alichofundisha huyu. Kwa hivyo, ninamna gani inashangaza kwa leo, wengine hujiitiliya nduguBranham bila kufuata kile alichotangaza kwa sehemu ya Mungu? Kwa wengine, hadithi ya Mhindi huyu ilikuwamuda yaonzuri ya pana mafundisho yao kwakitendo chalugha na kalamu yao. Kwa muda kama hizo, mafundisho zakidini ao hizo za kidunia, hufanya kila linalowezekanakuingiza jambo na kuzusha kutoaminiana kwa watu. Kunahata hivyo ingefanyika, kwa kila mmoja wetu, kuona kama mbele ya mlango yake mwenyewe hakuweza kugundua chochote cha kufagia.

Yeyote atakaesoma broshua hii kwa uangalifu atakuwa ameweza hakika wanatambua kwamba uwengi wa waamini wa wakati wetu wamekuwa wahusika wa upotevu, kupitiya udanganyifu wa kidini. Mtu hangeweza kusimamiya kwaile ambayo amehubiriwa tu. Kila mtu ana haki na wajibu wa kusoma Biblia katika roho ya maombi ili kupata nuru juu ya mambo yote kutoka kwa Mungu. Kuiga mara nyingi ni sawa na mfano wa asili kwamba sivyotu kwa msaada wa Mungu tunaweza kutofautisha.

Taifala Mungu, rudini kwenye Neno! Pokea nuru ya Roho Mtakatifu na unyenyekee chini ya mkono wenye nguvu wa Mungu, kwakuwa huongoza tena katika Kweli yote. Anaongoza kwenye njia ya haki, kwa ajili ya neno lake. Anatupa maarifa sahihikwa wakati ufaao. Kwa hiyo tukikesha, kuomba, naikiwa tunashimama kwenye mpaka ya Neno, tukilihesabu peke yake kuwa halali, hatuta ogopa kuanguka katika makosa, iwe wazi au siri. Kila tafsiri inapotokeya katika Neno – haijalishi ni nani anayeitoa. Paulo anaandika hivi: ***"Ikiwamtu anakutangazia Injili nyingine … na alaaniwe!"*** (Gal. 1:8) Hebu turudi kwenye Biblia! Turudi kwenye Injili isiyochanganywa. Na ipendezwe na Mwenyezi Mungu kutuma watumishi waaminifu katika shamba la mzabibu wake; ya wale

wanaohubiri Injili kamili kwauvuvio na chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Wawe watu watangazao mashauri yote ya Mungu, na wawe watumishi wa Mungu wenye ushimamizi mbele yake ya kutoongeza wala kupunguza chochote kwa ushuhuda wa Maandiko Matakatifu.

Waamini leo hawapaswi tena kujiruhusu kuwachini ya ulelezi, lakini wafanye kila kitu ili kufikia kimo cha mtu mkamilifu ndani ya Kristo. Wanapaswa kujijulisha wao wenyewe na kuhukumu kile kinacho hubiriwa.

Kwa neema ya Mungu, nilipata uwezo wa kuleta Nenokatika nchi arobaini tofauti kwa idadi kubwa ya watu ambao waliongozwa kwakilindi ndani ya neno lake. Wengi wao walikuwa na uzoefu mpyapamoja na Mungu na kutambua kile ambacho Mungu alikuwa akifanya katika wakati wetu. mimi sifungwe kwenye shurti ya kanisa fulani ao zehebu fulani, lakini ninabeba jukumu mbele za Mungu kuleta Neno Lake kwa watu Wake, kama alivyoliacha kwetu kama urithi.

Tafsiri za mahubiri ya Ndugu Branham zimeleta kwa watu wengi baraka kubwa. Yeye ni zaidi ya hayoalitambua kwa ujumla jinsi ndugu Branham alibarikiwa na kutumikishwa na Mungu. Ni yule tu asiyemtakia mema yeye mwenyewe aukwa wengine, na anayekataa Maneno na matendo ya Mungu katika hiiwakati kwa kukataa kutambua uthibitisho wa Neno Lake, yule ndiye atakaye pita pembeni ya yale ambayo Mungu anafanya. Kurudi kwa Yesu Kristo kumekaribia, na ndiyo sababu tunapaswa kuchukuakwa umakini Neno na maahadi za Mungu kwa wakati wetu. Utume yangu sio tu kusema juu ya „Mwokozi mpendwa“ anayeokoa wenye dhambi na kuponya wagonjwa. Mnamo mengi ya kuifanya. Wito wangu ni kutangaza neno lakinabii na kugawa chakula cha Mungu kwa wakati huu, nahili kwa kuwajulisha mashauri yote ya Mungu. Kwakiasili wokovu wa nafsi unathibitishwa ndani ya hayo.

Daima kwakufanya mazowezi mapya BWANA huthibitisha Neno lake, huokoa wenye dhambi, huponya wagonjwa nakuwakomboa

waliofungwa. Yeye yuko na anabaki Yule Yule Jana, leo na hata milele. Nguvu ya Neno Lake, ya Damu yake na ya Roho wake bado ni ile ile. Hii ndiyo sababu sisitunaweza kufikiya thibitisho ile ile katika wakati wetu. Bwana, kwa uaminifu Wake, aliongoza hivyo kazi hii ya umishonari, maelfu ya watu wamepokea baraka kubwa, Mashariki na Magharibi, Kusini na Kaskazini.

Tutaendelea, kwa msaada wa Mungu, kufanya yote yaliyo ndani ya uwezo wetu wa kuwatumikia watu wa Mungu. Neno ambalo Mungu alilo funuwa, akilitangaza kwa kinywa cha mtumishi wake na nabii William Branham, lazima ligabuliwe kwa wa watoto wote wa Munguwa wakati wetu. Ujumbe wa wakati wa mwisho unaongoza watu wengi kuchukua muda wa maombi na kusoma Biblia. Wengi wametambuwa kwamba chochote Ndugu Branham alicho fundisha kinapatana kamilifu na Neno la Mungu. Hatukufwasa hadisi za watu, bali sauti ya Mchugaji Mwema, ambalo linaambiwaupya wale waliyo wake, wa siku zetu, kupitiya neno lililo funuliwa. Yule anayeishi kweli ndani yauwepo wa Mungu anaamini Neno lililo funuliwa, kuthibitishwa, likitimizwa sasa na Roho Mtakatifu. Yesu Kristo ni yeye yule, na leo tena, Yeye anazungumza na Walio Wake na kujidhihirisha Mwenyewe kwao. Yeye anayeishi katika uwepo wake pia anaishi katika mambo anayofanyakwa sasa.

## Tangazo

Baada ya kukatiza matangazo ya redio, imewezekana kwangu kuyaendeleza tena. Barua nyingi kutoka Ulaya Mashariki na Magharibi na sala nyingi za waliotawanyika zimeonyesha jinsi usambajazi hio imekuwa ya muhimu na yenye kuimarisha imani.

Tutaendelea, kwa msaada wa Mungu, kufanya yote tuwezayo kuwatumikia watu wa Mungu. Neno lililofunuliwa na Mungu, lililotangazwa kwa kinywa cha mtumishi na nabii wake, William Branham, linapaswa kusambazwa kwa watoto wote wa Mungu kwa wakati huu. Ujumbe wa wakati wa mwisho uliwafanya wengi

kuchukua muda wa kuomba na kusoma Biblia na kugundua kwamba kila kitu Ndugu Branham alifundisha kinalingana na Neno la Mungu. Hatukufuata hekaya zilizotungwa kwa werevu, bali sauti ya “Mchungaji Mwema” ikinena kupitia Neno Lake lililofunuliwa kwa walio Wake katika wakati huu. Yeye anayeishi kweli katika uwepo wa Mungu huamini Neno lililofunuliwa sasa, lililothibitishwa na kutimizwa na Roho. Yesu Kristo ni yeye yule. Hata sasa anazungumza na kujidhihirisha kwa walio Wake. Yeye anayeishi katika uwepo wake anaishi katika kile anachofanya sasa.

**1933 – 1973**

Kama vile sauti ya baragumu kuu, Ujumbe ya wakati ya mwisho ilisikika kwenye bara zote hadimwisho wa dunia. Mnamo Juni 11, 1973, itakuwa miaka 40 tangu MunguMwenyezi alimutuma mtumishi wake na nabii William Branham,

akimwambia kupitia Nguzo ya Moto, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kama mutangulizi wa kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, hivyo ndivyo unavyotumwa na ujumbe kabla ya kuja kwake kwa pili ”.

Bwana awabariki wale wote ambaowametambua"leo" yao, na ambao wana shiriki kwa kazi ya Mungu kwa wakati huu.

Anae tenda kwa upande wa Mungu

Br. Frank

Ikiwa unapendezwa kupokea vitabu vyetu,
waweza kutuandikia kupitia anwani ifwatayo:

Kituo cha Misheni
Sanduku la Posta
100707 47707 Krefeld, Ujerumani

Waweza kuingia kwenye mtandao wakati wa mikutano yetu ya wikendi ya kwanza ya mwezi. Siku ya Jumamosi Jioni pa saa 19:30 h (Saa ya kati ya Ulaya), Jumapili asubuhi pa saa 10:00 h. Mikutano ya weza kusikilikana katika Lugha 13 tofauti duniani pote.

Pokeeni sehemu kwa yale ambayo Mungu anayo yafanya sasa kulingana na mpango wake wa okovu!

Ukurasa wa vuti: http://www. freie-volksmission. de

Barua pepe: volksmission@gmx. de

Fax: +49-2151/951293

or

Ukurasa wa vuti: https://www.misia.sk

Barua pepe: gospel2nations@misia.sk

Tel: +256(0)786 892 319, (0)758 023 639,(0)775 283 810

Na mwandishi na mchapishaji E. Frank